**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA PILI WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

# SOMO: SAYANSI [05]

**TAREHE 04/05/2021 MUDA: SAA 1:30**

**JINA LA MTAHINIWA:** ______________________________________________

**JINA LA SHULE:** ________________________________________________________

**WILAYA**: ____________________ **MKOA:** ____________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

**SEHEMUA: chagua herufi ya jibu sahihi**

1. Ni kundi lipi la udongo kati ya yafuatayo huwa na tabia ya kushikamana?
   a. Udongo wa kichanga b. udongo wa tifutifu c. udongo wa mfinyanzi
   d. udongo wenye vipande vya miamba laini e. udongo wenye mchanganyiko
2. Kitendo cha maji kusafiri kutoka kwenye myeyuko hafifu kwenda kwenye myeyuko mzito huitwa:
   a. Mtiririko wa maji taka b. maada c. difyusheni d. osmosisi e. kuganda kwa maji
3. Moto unaotokana na vimiminika vinavyolipuka na kuwaka mfano mafuta ya petroli upo katika daraja gani? a. A b. F c. D d. B e. C
4. Ugonjwa wa ngono unaosababishwa na bakteria aitwaye Neisseria ni upi kati ya yafuatayo?
   a. VVU b. kisonono c. pangusa d. kaswende e. trichomonasi
5. Waya unaounganishwa na mtaimbo wa shaba wenye urefu wa takribani mita moja ambao huchimbiwa chini ya ardhi hujulikana kama waya wa-
   a. Sakiti b. ethi c. umeme d. chaji e. laivu
6. Moja ya sababu ya vyura kujificha kwenye udongo wakati wa kiangazi ni-
   a. Kuzuia upotevu wa maji mwilini b. kujiepusha na maadui c. kutaga mayai
   d. kujivua ngozi e. kupoza mwili kutokana na joto
7. Mirija ya falopia katika uzazi wa mwanamke huunganisha sehemu mbili ambazo ni _____ na ___
   a. Uke na ovari b. shingo ya kizazi na uterasi c. shingo ya kizazi na ovari
   d. uterasi na uke e. ovari na uterasi
8. Kwa nini samaki huweza kuogelea kwa urahisi kwenye maji?
   a. Ana mkia mrefu b. ana umbo la kuchongoka c. ana magamba magumu
   d. ana matamvua mengi e. ana mapezi laini
9. Zipi ni sifa kuu za mammalia?
   a. Kutaga mayai, damu moto na kunyonyesha
   b. Kuishi nchi kavu, damu baridi na kupaa hewani
   c. Kuwa na nywele, kunyonyesha na damu moto
   d. Kuishi majini, kutaga mayai na kula nyasi
   e. Kunyonyesha, damu baridi na kuwa na nywele
10. Ukuaji wa mtoto ndani ya mfuko wa uzazi huchukuwa muda gani mpaka mama mjamzito anapojifungua? a. Siku 9 b. miaka 9 c. miezi 8 d. miezi 9 e. siku 90
11. Gesi inayo zalishwa na bakteria wanaoozesha taka katika mazingira yasiyo na hewa ya oksijeni huitwa a. Gesi vunde b. gesi ya kabondayoksaidi c. mboji d. gesi mkaa e. gesi ya naitrojeni
12. Kwa nini mafuta ya taa huelea juu ya maji?
    a. Maji ni mepesi b. densiti ya maji ni ndogo c. densiti ya mafuta ni ndogo
    d. densiti ya mafuta ni kubwa e. densiti ya maji ni sawa na densiti ya mafuta
13. Kifaa au sehemu maalumu inayotumika kuteketeza taka kwa kutumia joto kali huitwa__
    a. Kemikali b. moto c. mashine ya moto d. shimo la taka e. tanuri
14. Upi kati ya magonjwa yafuatayo husababishwa na virusi?
    a. Kifua kikuu b. kipindupindu c. malaria d. surua e. trakoma
15. Nini kazi ya uti wa mgongo?
    a. Kutengeneza uroto katika mifupa b. hushughulikia matendo yasiyo ya hiari
    c. hushugulikia matendo ya hiari d. hutumika katika kufikiri
    e. ni sehemu ambapo neva za fahamu hutengenezwa
16. Ni mimea ipi kati ya ifuatayo inaweza kuongeza chumvichumvi za naitreti katika udongo?
    a. Mihogo na miembe b. mhindi na mharagwe c. mikunde
    d. mbaazi na mahindi e. karanga na kabichi

17. Ni madhara gani huweza kutokea kama mtu hatazingatia alama hii?



a. Ataambukizwa magonjwa b. anaweza kuungua moto c. anaweza kupata magonjwa ya ngozi na kansa d. anaweza kupata ajali e. anaweza kuteleza na kuanguka

18. Ili chuma kiweze kupata kutu lazima kuwepo na vitu gani?

a. Maji na asidi b. maji na besi c. maji na kabondayoksaidi
d. oksijeni na chumvi e. maji na oksijeni

19. Viumbe hai wanatabia zifuatazo isipokua:

a. Kuzaa na kupumua b. kujongea nakuitikia vichochea c. kukua na kujongea
d. kunyonyesha na kula e. kuhisi na kula

20. Kwa nini ni vigumu kukiona kitu kilichopo nyuma ya ukuta?

a. Kwa sababu mwanga unasafiri katika mstari ulionyooka
b. Kwa sababu mwanga una kasi kuliko sauti
c. Kwa sababu mwanga unasafiri katika mawimbi
d. Kwa sababu sauti husafiri kwa kasi kuliko mwanga
e. Kwa sababu mwanga hautoshi

21. Nini kitatokea iwapo mimea haita kuwa na klorofili?

a. Mimea haitapata maji b. mimea haitatengeneza chakula c. mimea itakua haraka sana
d. mimea haitakuwa na nguvu e. mimea itakuwa na mizizi dhaifu

22. Mtu anayeumwa ugonjwa wa malaria damu yake ikichunguzwa kwa kutumia darubini itaonekana na vimelea vinavyoitwa________

a. Virusi b. fangasi c. bakteria d. plasmodiamu e. mbu

23. Ni tendo gani linaweza kutumika ili kutenganisha maji na chumvi?

a. Kufukiza maji b. kusafisha maji c. kumwaga maji d. kulainisha e. kumimina chumvi

24. Ipi kati ya zifuatazo sio kazi ya damu?

a. Kusafirisha taka mwilini b. kusafirisha gesi c. kusafirisha chakula
d. kurekebisha joto la mwili e. kumeng'enya chakula

25. Zipi kati ya maada zifuatazo zipo katika hali yabisi?


a. Mekyuri, barafu na mchanga b. barafu, sukari na hewa c. hewa, mvuke na maji
d. damu, jiwe na maziwa e. karatasi, barafu na plastiki

26. Zifuatazo ni tabia za badiliko la kiumbo isipokuwa:

a. Huweza kurudishwa na kuwa katika hali yake ya mwanzo
b. Uzito haubadiliki
c. Kitu kipya hupatikana
d. Hakuna joto wala mwanga unaozalishwa
e. Hakuna kitu kipya kinachopatikana

27. Kipi katika ya vitu vifuatavyo huweza kupitisha joto kwa urahisi?

a. Chuma b. ubao c. glasi d. plastiki e. hewa


28. Alama  katika sakiti ya umeme huonesha nini?

a. Swichi b. waya c. kikinzani d. fuzi e. betri

29. Yapi kati ya magonjwa yafuatayo unaweza kuyapata iwapo hutasafisha vyoo na jiko?

a. Trakoma na UKIMWI b. malaria na minyoo c. kichocho na fangasi d. kuhara na kipindupindu e. kichocho na minyoo

30. Nini thamani ya herufi ya "R" katika mchoro ufuatao?




a. m 2 b. m 20 c. m 40 d. m1 e. m 4

31. Ni kitu gani hupotea kwa wingi mtu anapoharisha?
a. Vitamini b. protini c. maji d. hewa e. mafuta


32. Ni kwa nini watu wanaoishi na VVU wanahitaji vyakula vyenye virutubisho zaidi?
a. Wanapata njaa kila siku b. ugonjwa wao ni wa muda mrefu c. maisha yao ni mafupi
d. wanahitaji kunenepa Ili kuepuka unyanyapaa e. wanahitaji kuimarisha kinga ya mwili

33. Moja kati ya njia zifuatazo hazienezi virusi vya UKIMWI:
a. Kuchangia damu yenye virusi b. kuumwa na mbu c. kuchangia sindano
d. ngono zembe e. kuchangia miswaki

34. Ni hatua gani muhimu hufuata baada ya kubuni dhanio katika jaribio la kisayansi?
a. Kukusanya data b. kufanya jaribio c. kubaini tatizo d. kuchanganua data e. kuandika ripoti

35. Zipi ni hatua tatu za mwisho katika uandishi wa ripoti?
a. Lengo, vifaa, matokeo b. njia, lengo, hitimisho c. njia, matokeo, hitimisho
d. matokeo, vifaa, lengo e. kichwa, lengo, vifaa

36. Aina hii ya antena huitwa:
a. antena mchirizo akisi
b. antena kidoa
c. antena safu
d. antena honi
e. antena waya



37. Antena ambazo hutokana na muunganiko wa antena nyingi ambazo hufanya kazi kwa pamoja kama antenna moja huitwa:
a. Antena kidoa b. antena akisi c. antena safu d. antena kipenyo e. antena waya


38. Zifuatazo ni faida za matumizi ya barua pepe isipokuwa:
a. Husafirisha virusi b. ni rahisi kutuma c. kushirikishana taarifa d. humfikia mlengwa kwa haraka e. kupungua kwa gharama

39. Mojawapo kati ya hizi sio injini pekuzi:
a. Google b. yahoo c. bing d. majibu.com e. barua pepe

40. Katika kitabu kazi kwenye programu jedwali seli iliyochaguliwa kwa ajili ya kuingiza data au kurekebisha data huitwa: a. Seli amilifu b. pau seli c. menyu d. hifadhi kama e. hifadhi

**SEHEMU B: MAJIBU MAFUPI**

41. Chembechembe hai ya damu iliyooneshwa katika mchoro huu huitwa__________________



42. Tafuta kazi iliyofanywa na mtu ambaye alitumia kani nyutoni 15 kuvuta mzigo umbali wa mita 12

43. Acidi + metali $\longrightarrow$ chumvi + Q
Herufi Q huwakilisha nini?

44. Ni gesi ipi hupatikana kwa kiasi kikubwa kuliko zote katika anga?

45. Ni sehemu gani katika runinga hutumika kuonesha picha?